GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 **Awwal-ath'Than** 1445 **AH** **OKTOBA** 2023 **ZAHOOR** 1402 **HS** **BEI TSH 800/=**

Istighfar na Taubah

HABARI UK> 3

Maana ya kweli ya Istilahi hizi

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatihah, Khalifa Mtukufu Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] alisema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anakubali toba ya waja wake, kwa sharti kwamba iwe ni toba ya kweli na sio tu kutamka maneno.

Khalifa mtukufu[atba] alisema kwamba ndani ya Qur'ani Tukufu, imeelezwa kwamba Mwenyezi Mungu huwaruzuku wale wanaotubu kikweli kwa mali na vizazi, na inakuwa njia ya kuokolewa na ghadhabu ya



Hadhrat Ameerul Mumineen Hazrats Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih Wa tano[atba] akihutubia waumini katika Msikiti wa Baitul Futuh, Morden, London, Uingereza – Siku ya tarehe 04 Agosti 2023.

Shule ya Msingi Ahmadiyya wafanya Mahafali ya Wahitimu

Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, mgeni rasmi akiwa na Naibu Amir Sheikh Abid Mahmood Bhutti Sahib



Kwa fadhili na Baraka za Allah na khilafat -e-Ahmadiyya Shule ya msingi Ahmadiyya iliyopo Kihonda katika Manispaa ya Morogoro ilifanya mahafali ya wahitimu wa darasa la saba mwaka huu 2023 kwa amani na utulivu mkubwa.Mgeni rasmi katika mahafali hayo alikuwa ni Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib Amir na mbashiri mkuu nchini Tanzania. Hafla hiyo ilifanyika siku ya Alhamisi tarehe 07/09/2023 kuanzia saa 3:00 asubuhi. Hafla ilianza kwa

HABARI UK> 4

>UK .4 Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Istighfar na Taubah >UK .8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Kurani Tukufu

Moyo daima dawamu, unapupa ya kubusu kitabu kitakatifu na kufanya towafa kuzunguka Kuruani Tukufu, kwani hiyo ni Qaaba yangu. (Seydina Ahmad[as])

Wasomaji wa vitabu hukimbilia kumfahamu mwandushi wa kitu hicho. Je? Umewahi kuandika kitabu kingine na kitabu hicho kilipokelewa vipi. Wasomaji. Na usomaji wa Kurani Tukufu akija na fikra basi tunampa pole kwani atakuwa kama yule anatarajia anaetarajia mkaa kutoka kwenye mgomba. Hapa tumeingia ulimwengu mwingine. Muujiza wa kwanza wa Kurani Tukufu iliyoteremshwa takribani miaka ishirini na mbili (610-632) haina desturi ya wewe kukutana na jina la Mtunzi hutalikuta. Ni kitabu pekee ambacho hakina Mtunzi kama tulivyozoea kwamba, watu walikaa wakachagua baadhi ya mambo na wengine wakayaweka kando. Hapa pana haja ya kutafakari.

Ni desturi pia ya kwamba, mwandishi hutoa shukurani kwa waliomsaidia na pili hukiri udhaifu wake na kutoa ahadi ya kufanya marekebisho katika chapa inayofuata. Katika Kurani Tukufu hakuna msururu wa wasaidizi wala kukiri udhaifu. Tunachokiona nao pia ni muujiza. Tunahakikishiwa toka mwanzoni kwamba tuondoe shaka kabisa kwani kitabu hiki nimekiteremsha mwenyewe Mwenyezi Mungu nijuaye sana. Nijuae sana. Ninaweza kuelewa ukisema nijuae lakini kusema nijuaye sana haiwezi kuwa kauli ya Binadamu ambaye Mshairi mmoja aliwahi kusema Binadamu ni dhaifu tena ni dhaifu sana" ni dhaifu wa kila kitu ukiwa ni ubongo pia.

Muujiza mwingine wa Kurani Tukufu ni kwamba daima unatoa ushahidi wa madai yake. Daima falsafa ya mafundisho yake. Hailazimishi bali inashawishi. Kuonesha kuwa Mwenyezi Mungu ajuaye sana. Tumehakikishiwa kuwa hakuna kosa lolote katika kitabu hiki. Mambo mawili yanajitokeza. Toka Kuruani Tukufu iteremshwe hakuna kosa lolote liwe katika maumbile, falsafa, hisitoria sayansi ambalo limeonesha kwamba Kuruani Tukufu (Allah apishe mbali) imekosea. Yote yametimia yanaendelea kuushtua ulimwengu ilikuwaje mtu wa Jangwani huko uarabuni miaka 1400 iliyopita kuyafahamu yote hayo. Kisa cha Nzi aliyeanguka kwenye Maziwa na ukanywa bila shida yoyote. Ni jambo ambalo linakubaliwa hivi sasa na Wanasayansi. Allah ametoa ahadi ya kulinda uteremsho huu. Wachunguzi na watafiti wa kila aina wamepata vipawa wakizama na kuibuka ili kutafuta kasoro yoyote au neno lililoingia katika kitabu kitakatifu. Angalau kwa hili wamekuwa wa kweli hata silabi moja haijabadilika.

Tukishayafahamu yote hayo, nini imekuwa shabaha ya kuteremshwa Kuruani Tukufu, hiki hasa ni kii na shabaha kuu. Sote tunafahamu umuhimu wa kitu ni kutimiza shabaha ya kutengenezwa kitu husika. Kitabu cha kimbingu kina kazi ya kuwatoa katika maisha ya dhambi, kuwatakasa na kuwapa uwezo wa kumtambua Allah na kujenga uhusiano wa Allah. Mapenzi hayo ndio mzizi wa wokovu na hio ndio pepo ambayo ukiingia hakuna kuchoka au kusikia maumivu. Na kitabu hicho na kitabu hicho humuondolea Kila aina ya mashaka na kumpa uelewa kiasi kwamba anamuona Allah. Ni lazima kuanzisha uhusiano baina ya Allah na Mja. Kiasi hiki Mja awe mtumishi wa Allah. Kitabu kikishindwa kutimiza wajibu huu ambao kwa hakika ndio shabaha yake na kianze kutoa visingizio vingine, hiyo itakuwa kama mgonjwa aliyeitwa kwa Daktari na anaombwa amtibu mgonjwa na Daktari anasema hawezi kumtibu anajua mieleka, falsafa hapana shaka, huyu ataitwa Juha msanii na atalaumiwa na watu wote wenye ..... Kitabu cha Allah na Mtume saw kinawatoa Binadamu katika tope la dhambi na kuanzisha mahusiano wataharibu baina ya Allah na Dunia.

Historia inashuhudia ukweli huo. Waislam waliokuwa duni, walioshinda virabuni, magomvi yasiyokwisha, wakapata makosa wakang'aa, wakaeleza nuru duniani, wakakesha kwa Dua za vilio na dunia ikanusurika kutokana na wao. Lakini mapinduzi hayo yalitoka wapi? Yalitokana na kuipenda, kuienzi, kuisoma na kutekeleza mafundisho ya Kuruani Tukufu. Uzima, uhai, maendeleo ya Binadamu yamo katika Kurani Tukufu. Matatizo tuliyonayo ya unyonyaji hivi leo, ukoloni mambo leo, uhasama wa kidini, matatizo ya tabia nchi, vita kuonewa kwa matabaka fulani katika jamii. Yote hayo anatueleza Khalifa wa V Hazrat Mirza Masroor Ahmad atba kuwa yatakuwa historia tukiifuata Kurani Tukufu kama walivyofanya maswahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad saw na siku zote tukumbuke na tuzingatie kuwa kusema bila kutenda ni chukizo kubwa kwa Allah.



QUR'AN TUKUFU

17_.SURA__BANII__ISRAAIIL

24. Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu ye yote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao au wote wawili wakifikia uzee pamoja nawe, katu usiwaambie neno lo lote lenye kuashiria kwamba umechukia wala usiwakemee, bali zungumza nao kwa maneno ya ukarimu.

وَقَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا ؕ اِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ اَحَدُهُمَآ اَوْ كِلٰهُمَا فَلَا تَقُلْ لَّهُمَآ اُفٍّ وَّلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيْمًا ﴿۲۴﴾



NUKUU YA HADITHI

(Sahih Muslim, Kitabul Birr Wassilatul Hadith No.6510)

Imesimuliwa na Hazrat Abu Hurairah[ra]. Kwamba Mtume[saw] alisema: Mwenye bahati mbaya (na kurudia maneno hayo mara tatu) ni yule aliyewakuta wazazi wake wote wawili au mmoja wao katika uzee kisha hakuweza kuingia Peponi (kwa sababu ya kutokuwatendea vizuri).

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ عَنْ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ رَغِمَ أَنْفُ ثُمَّ رَغِمَ أَنْفُ ثُمَّ رَغِمَ أَنْفُ قِيلَ مَنْ يَا رَسُولَ اللَّهِ قَالَ مَنْ أَدْرَكَ أَبَوَيْهِ عِنْدَ الْكِبَرِ أَحَدَهُمَا أَوْ كِلَيْهِمَا فَلَمْ يَدْخُلْ الْجَنَّةَ –



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

"Mtu asiyewaheshimu wazazi wake wala asiyezitii amri zao maarufu, zisizo kinyume cha Quran Tukufu, wala hawatumikii kwa haki, hayumo katika jumuiya yangu." (Safina ya Nuhu, uk. 27)

"Kuwatumikia wazazi ni jambo moja la maana sana. Imesimuliwa katika Hadithi ya Mtume[saw] kwamba watu wawili wana bahati mbaya sana; wa kwanza ni yule aliyepata mwezi wa Ramadhani na ulipita lakini madhambi yake hayakusamehewa; na mwingine aliyepata wazazi wake na walifariki lakini madhambi yake hayakusamehewa. Mtoto anapokuwa chini ya kivuli cha wazazi basi huwa wanamtunza katika mambo yote. Endapo mwenyewe anajikuta katika mambo ya maisha basi huwa anaelewa thamani ya wazazi. Ndani ya Kurani Tukufu Mwenyezi Mungu ametoa kipaumbele kwa mama kwani mama huvumilia taabu nyingi kwa ajili ya mtoto; hata kama mtoto atakuwa amepata ugonjwa wa kuambukiza kama ugonjwa wa ndui, wa kuhara au wa tauni; mama hawezi kumwacha; na huwa anashiriki katika shida zote. Huu ni upendo wa asili ambao hakuna upendo mwingine unaoweza kushindana nao. Mwenyezi Mungu aliashiria ndani ya Kurani Tukufu ان الله يامر بالعدل والاحسان وايتاء ذى القربى (16:91) Yaani: Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu, na hisani, na kuwapa (kama uwapavyo) ndugu."

(Malfuzat, juz. 7, uk. 375)

"Hatua ya kwanza ya mtu kuwa mwenye bahati njema ni kumheshimu mama. Mara nyingi

Endelea Uk> 8

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Istighfar na Taubah

KUTOKA UK> 1

Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika tukio moja katika Qur'ani Tukufu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

Bila ya shaka wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, na Mwenye kurehemu. (Qur'ani Tukufu, 4:65)

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba, hata hivyo, sharti la hili ni kwamba mtu hakika atafute msamaha na atubu. Imeandikwa kwamba Mtukufu Mtume (saw) alisema wakati fulani kwamba kwa mtu ambaye ametubu kikweli, ni kana kwamba hakuwahi kukosea kabla. Mtu anakuwa salama kutokana na athari mbaya za kufanya dhambi. Kisha Mtukufu Mtume (saw) akataja aya ifuatayo:

"Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubia kwake na huwapenda wanaojitakasa" (Qur'ani Tukufu, 2:223).

Toba ya Kweli ni Nini?

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Mtukufu Mtume (saw) aliulizwa ni nini kinachohusisha toba ya kweli. Mtukufu Mtume (saw) alijibu kwa kusema majuto na huzuni. Ni katika kufanya hivyo ili mtu aweze kusamehewa dhambi zake na kufaidika na rehema za Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) ameainisha masharti ya toba ya kweli. Sharti la kwanza aliloeleza ni kuachana na mawazo mabaya na machafu. Haya ni mapambano makubwa ambayo mtu lazima ayafanye ili kufikia toba ya kweli.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba sharti la pili la toba ya kweli lililoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa (as) ni kwamba mtu lazima aonyeshe majuto na huzuni ya kweli. Ni lazima aelewe kwamba starehe na vivutio vya dunia hii ni vya muda tu, na kubakia navyo hakuleti manufaa yoyote.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba sharti la tatu lililoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa (as) kwa toba ya kweli ni kuazimia kwa uthabiti kutokaribia tena uovu huo. Hili lisiishie kwenye maazimio tu, bali ni lazima juhudi kubwa zifanywe kubadilisha matendo maovu kwa matendo mema na ya uchamungu.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba kuanguka katika uovu mmoja hupelekea mwingine, na kisha mwingine. Kwa hivyo ni muhimu sana kufikia toba ya kweli. Ni lazima tujaribu kuzitakasa nyoyo zetu na kufanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba hatukosi kamwe katika kutimiza haki zinazodaiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na zile zinazodaiwa na viumbe Wake. Ni sharti kwetu daima kutekeleza mafundisho ya Mwenyezi Mungu, Mtume Wake (saw) na Masihi Aliyeahidiwa (as) ili kutimiza lengo la kiapo chetu cha utii. Bila juhudi kuelekea toba ya kweli, kiapo chetu cha kujirekebisha kinageuka kuwa kitupu.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) amevuta mazingatio ya Jumuiya yake kuelekea kwenye toba ya kweli mara nyingi sana na kwa hakika, amechukua kila fursa kuangazia mada hii. Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba angewasilisha baadhi ya sehemu za Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu suala hili.

Faida za Kutafuta Msamaha

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as), ambaye alizungumza kuhusu faida ya kuomba msamaha. Alisema umma wa Kiislamu umepewa uwezo wa aina mbili; moja ni uwezo wa kupata nguvu, na pili ni uwezo wa kuonyesha kwa vitendo nguvu hizo. Nguvu inaweza kupatikana kwa kutafuta msamaha na kutafuta msaada. Kama vile watu wanavyofanya mazoezi kwa kunyanyua uzito na njia nyinginezo, kutafuta msamaha huimarisha nafsi na kukuza ustahimilivu wa moyo. Ghafar pia inahusu kufunika; hivyo, kwa kufanya istighfar - kutafuta msamaha - mtu hujitahidi kutiisha na kufunika zile hisia na shauku zinazomweka mbali zaidi na Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as), ambaye alisema kwamba bila shaka wanadamu wameumbwa dhaifu, kutokana na hilo kwa hakika watapungukiwa katika utimilifu wa amri fulani. Hii inafanya kuwa hakika kwamba Mungu bila shaka anakubali toba ya wale wanaotubu kikweli. Mtu anatakiwa kutubu kwa namna ambayo hata kama angetupwa kwenye moto, hatarudia tena kutenda uovu huo huo. Ni moja ya sifa kuu za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwamba anakubali toba ya kweli ya watu. Baadhi ya watu huuliza swali, je, kuna umuhimu gani wa kutubu ikiwa wanakwenda kukutana na hatima ya adhabu? Walakini, hii sio kweli. Kwa hakika, Mungu hukubali toba ya wale wanaotubu kikweli. Kwa kusema kwamba Yeye ndiye Mwenye kurejea kwa rehema na anakubali toba, Mwenyezi Mungu ametoa matumaini. Kama matumaini haya yasingekuwepo, basi watu wangewezaje kutubu? Kwa hiyo, toba ya kweli inaongoza kwenye kukubali toba.

Huduma ya Midomo tu haitoshi

Khalifa mtukufu (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba kuomba msamaha hakuwezi kuwekewa mipaka kwenye kutamka maneno tu katika kusujudu, bali lazima kuambatanishwe na juhudi na matendo ya kweli hadi mwisho wa kuepuka na kuondoa uovu kutoka kwenye maisha ya mtu.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as), ambaye alisema kwamba maafa yanayoikumba dunia ni njia ya kuvuta hisia za watu kwenye ongezeko la kutafuta msamaha.

Hadhrat Khalifatul Masih V (atba) alisema kwamba kwa kuzingatia hali za dunia ya leo na vita vikiwa ukingoni, sote tunapaswa kuongezeka katika kutafuta msamaha wa kweli. Kuna wale wanaosema kwamba wameomba msamaha mara maelfu, na hakuna kilichobadilika. Ilhali wanapoulizwa maana ya kuomba msamaha kikweli, wao hawajui. Kwa hivyo, mtu anapaswa daima kutafuta toba kwa moyo wa kweli, na kwa namna hiyo hiyo, kutafuta uwezo wa kufanya matendo mema katika siku zijazo. Vinginevyo, kutamka tu maneno ya kuomba msamaha hakuwezi kuwa na matokeo ya kweli. Badala yake, yale yanayosemwa na ulimi yanapaswa kuwa kielelezo cha kile kilicho moyoni kikweli. Hapo ndipo Mungu anaweza kuepusha dhiki na maafa kabla hayajafika.

Toba ya Kweli Huleta Mabadiliko Kamili katika Mtu

Khalifa mtukufu (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba baada ya kuweka kiapo cha utii kwake, ikiwa mtu anaendelea kumtendea mke wake sawa, au namna anavyowatendea watoto wake inabakia vile vile, basi kiapo chake cha utii hakina thamani. Badala yake, baada ya kufanya Baiat, mtu anapaswa kuonyesha mfano kwa namna ambayo unawaongoza wengine kushuhudia kwamba mabadiliko ya kweli yametokea ndani ya mtu huyu. Hivi ndivyo hasa matokeo ya toba ya kweli yanavyopaswa kuwa.

Kuomba Msamaha kwa Mitume

Khalifa mtukufu[atba] alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa[as], ambaye alinukuu riwaya ambayo Mtukufu Mtume[saw] alilia na kisha akawahutubia watu akisema kwamba misiba imeshikamana na kila mtu kama wadudu chungu, na njia pekee ya kuokolewa kutoka kwenye misiba hiyo ni kwa toba ya kweli. Masihi Aliyeahidiwa[as] aliendelea kusema kwamba baadhi ya makuhani wa Kikristo wametoa madai yasiyo na msingi kwamba kwa vile Mtukufu Mtume[saw] pia alikuwa akiomba msamaha, hivyo inaonyesha kwamba alikuwa ni mwenye dhambi, Mungu apishe mbali. Masihi Aliyeahidiwa (as) alijibu kwa kusema kwamba watu kama hao hawatambui kwamba kutafuta msamaha au istighfar ni sifa ya hali ya juu. Wanadamu wameumbwa na mapungufu ya asili, na manabii wanatafuta msamaha ili wasianguke kwenye udhaifu huo wa

Endelea Uk> 5

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Kutoka toleo lililopita

(3) YESU KUPELEKWA NA ROHO MTAKATIFU KWA SHETANI NYIKANI.

Jambo hili la kupelekwa Yesu kwa shetani na ROHO MTAKATIFU ndio uthibitisho uliojitosheleza na kubainika kabisa kwamba ni njozi, kwa sababu Mungu aliye Mtakatifu Amtume Roho Mtakatifu kumpeleka Yesu kwa shetani tena nyikani mpendwa wake, tena aliyependezwa nae jambo hili haliingii AKILINI. Na haliwezekani.

Ni jambo lisilowezekana, kwa sababu SHETANI na MUNGU ni mahasimu wakubwa na hakuna kinachotazamiwa kutokea kwa mtu anayefuatana na shetani ila ni upotevu tu.

Maandiko kwenye vitabu kadhaa yamerekodia tukio la Adamu na mkewe kwamba, pindi walipokaa na SHETANI kwa muda wa dakika chache tu, matokeo yake yalikuwa ni kupotezwa wote sembuse siku arobaini. !!

(4) KUONGOZWA NA SHETANI NYIKANI.

Hivi ni nani asiye juwa kwamba kuongozwa na shetani ni tatizo kubwa kiimani, na kwa jamii, kwa sababu SHETANI ni mbaya mharibu imani na familia za watu zilizotulia. Ni nani asiye juwa hatari ya kuandamana na shetani? Dini ya Islam imefundisha kwamba, kila wanapoandamana japo watu wawili, basi mmoja lazima awe kiongozi wa dhidi ya yule mwingine, la sivyo, shetani atashika usukani na kuwaongozeni.

YESU mwenyewe kwa kuijuwa hatari ya kuwa pamoja na shetani, hofu yake inaonekana pale tu petro alipowaza mambo yasiyoendana na imani. Kwa mawazo tu mabaya ya Petro, alionekana ni SHETANI machoni pa Yesu, hivyo kumfukuzilia mbali?

Biblia inasema:

Akageuka, akamwambia Petro, Nenda nyuma yangu, Shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.(Mathayo 16:23)

Hiyo ilikuwa baada tu ya Petro kukosa kufikiria ya MUNGU na kuwaza ya binadamu. Akawa ni kikwazo kwake na akasema hana ushirika hata kidogo na watu wa sampuli hiyo. Ndio kusema kwamba, kama yale maandiko ya Yesu kupelekwa nyikani na kuketi pamoja na shetani, bali shetani kuwa na uwezo wa kumpeleka Yesu kokote atakako kwa masiku yote yale, ilikuwa ni kwa dhahiri, basi kwa nini auogope ushetani mdogo tu wa Petro na kutamani kanisa aondoke mbele yake?

(5) KUFUNGA SIKU AROBAINI MCHANA NA USIKU.

Habari hii pia inazidi kukozesha hoja kwamba, kwa hakika safari ya Yesu nyikani haikuwa ya kidhahiri bali ilikuwa ya kinjozi. Tunasema hivyo kwa sababu haijapata kuripotiwa katika historia kwamba kuna watu walifaradhiwa ibada ya kufunga hadi USIKU !!

Hii ni ibada ya ajabu ambayo haijulikani ilifundishwa na Nabii gani !!

Mara zote tunaona kwamba, manabii wanafundisha vitu ambavyo wao wenyewe wanakuwa mstari wa mbele katika kuvitekeleza. Kwa hiyo bwana Yesu akifundisha namna ya kufunga alisema:

«Tena mfungapo, msiwe kama wanafiki wenye uso wa kukunjamana; maana hujiumbua nyuso zao; ili waonekane na watu kuwa wamefunga.

Bali wewe ufungapo, jipake mafuta kichwani

unawe uso; ili usionekane na watu kuwa unafunga, ila na Baba yako aliye sirini; Na Baba yako aonae sirini atakujazi. Mathayo 6:16--18;

Kama ibada ya funga ilitakiwa hadi USIKU, hofu ya Yesu kwa wanafunzi wake ilikuwa ya nini?

Maana akili inakataa kabisa kuruhusu kumdhani Yesu hakujuwa kwamba kwa kawaida kila mtu huwa analala nyumbani kwake.

Kwa hiyo maelezo aliyoyatoa kuhusu funga na kile kinachoonekana kwenye simulizi ya Mathayo 11-4:1 ni tofauti kabisa na inadhihirika kwa hakika ilikuwa njozi. Kufunga ni mchana pekee, ambapo mnafiki anapata nafasi ya kukutana na watu mbalimbali kwenye harakati za maisha na hapo ndipo ili kujionesha kuwa amefunga, uso wake anataka uwe umekunjamana; kujiumbua nyuso zao; kama Yesu Alivyosema.

Kwa hivyo funga zake za kawaida lazima zilikuwa ni kama hivyo alivyotoa maelezo ya namna ya kufunga. Kwa maana USIKU alikuwa akipata huduma kama kawaida na malaika, (Marko 1:13)

Na neno swaumu (kufunga) maana yake ni «kujizuia» kufanya uovu wa kumchukiza Mungu, imefafanuliwa vizuri zaidi na Isaya pale aliposema:

Je! Kufunga namna hii ni saumu niliyoichagua mimi? Je! Ni siku ya mtu kujitaabisha nafsi yake? Ni kuinama kichwa kama unyasi, na kutanda nguo za magunia na majivu chini yake? Je! Utasema ni siku ya kufunga, na ya kukubaliwa na Bwana?

Je! Saumu niliyoichagua, siyo ya namna hii? Kufungua vifungo vya uovu, kuzilegeza kamba za nira, kuwaacha huru walioonewa, na kwamba mvunje kila nira?

Je! Siyo kuwagawia wenye njaa chakula chako, na kuwaleta maskini waliotupwa nje nyumbani kwako? Umwonapo mtu aliye uchi, umvike nguo; wala usijifiche na mtu mwenye damu moja nawe?

Ndipo nuru yako itakapopambazuka kama asubuhi, na afya yako itatokea mara; na haki yako itakutangulia; utukufu wa Bwana utakufuata nyuma ukulinde.

Ndipo utaita, na Bwana ataitika; utalia, naye atasema, Mimi hapa. Kama ukiiondoa nira; isiwepo kati yako, wala kunyosha kidole, wala kunena maovu;

na kama ukimkunjulia mtu mwenye njaa nafsi yako, na kuishibisha nafsi iliyoteswa; ndipo nuru yako itakapopambazuka gizani; na kiwi chako kitakuwa kama adhuhuri.

Naye Bwana atakuongoza daima, ataishibisha nafsi yako mahali pasipokuwa na maji, na kuitia nguvu mifupa yako; nawe utakuwa kama bustani iliyotiwa maji, na kama chemchemi ambayo maji yake hayapungui.

Na watu wako watapajenga mahali palipokuwa ukiwa; utaiinua misingi ya vizazi vingi; nawe utaitwa, Mwenye kutengeneza mahali palipobomoka; na, Mwenye kurejeza njia za kukalia. (Isaya 58:5 -12)

Kwa maana hiyo kufunga kunakosemekana kuwa YESU alifunga USIKU na MCHANA, ilikuwa ni kwa maana hiyo ya alijizuia kufanya madhambi usiku na mchana kama yanavyo bainisha maandiko alimkatalia SHETANI, yote aliyomshawishi, na ilikuwa akikesha kufanya ibada za usiku kule Gethsemane. ingawa wafuasi wake walilala fofofo,

na anayekataa ushahidi huo hapo juu basi afunge MCHANA NA USIKU kwa muda wa siku hizo arobaini bila ya kula chochote kama hatazikwa. Imesemwa ukiwa na IMANI kama punje ya haridali inawezekana.

Lakini hapo hapo kabla ya kufunga hizo siku arobaini mtu huyo anatakiwa asome kifungu hiki cha maneno ya Biblia.

«Kwa maana mjinga huamini kila neno» Mithali 14:15 -16,

Wajinga hurithi upumbavu mithali 14:18;

(6) KUBADILI JIWE UWE MKATE.

Tendo la kubadili jiwe kuwa mkate ilikuwa Yesu amaoneshwa jinsi wafuasi wake watakavyojihusisha kwenye maisha ya udanganyifu mkubwa, kiasi cha kuufanya udanganyifu huo kuwa ndio kiini cha dini ya kikristo. Kwa kawaida tunaona udanganyifu hufanywa na mwana mazingaombwe ili aweze kumudu gharama za maisha ya DUNIA kwa hila mbaya. Ndio kusema kwamba, mambo hayo hufanywa na mtu muongo na shetani kama vile Beelzebuli ambaye YESU alikataa kufananishwa naye.

Kwa sababu Yesu hakupenda maisha ya DUNIA. kama hoja ni kuonyesha miujiza, basi huonyesha kwa kuwepo kwa vitu halisi kama alivyoonesha makutano waliposhikwa na njaa. Kwamba aliletewa samaki halisi wawili na mikate halisi mitano akaiombea na hivyo kutosha kuliwa na watu zaidi ya elfu tano bila ya hesabu ya wanawake na watoto.

Kwa hivyo tukirejea kwenye kisa cha njozi ya Yesu kuona maono kama vile amekutana na shetani ilhali Yesu ni mwenye njaa kali na shetani kumpa akili ya kujiponya njaa hiyo kwa kufanya mazingabwe ya kugeuze jiwe kuwa mkate, ni wazi hapo alikuwa anafahamishwa tabia ya wafuasi wake itakavyokuwa. uwongo utakuwa ndio sehemu yao ya kujipatia mafao ya DUNIA, ndio maana hali hiyo leo tunaiona imejaa makanisani na kwa wachungaji. Na ili waendelee kufanya maongo hayo bila ya hofu yoyote, na pia mamuma wao yeyote asiwe na swali lolote kwao, ukatengenezwa uongo wa kupenyeza Bibliani aya zinazolinda madudu yao. Ndipo pale wanapodiriki kufuta sheria za Musa kwa kigezo kuwa eti «huwezi kuhesabiwa haki kwa kuifuata sheria» kupunguza amri kumi na kuacha nne tu, Na kuwauzia vyeti vya toba ili wapate ufalme wa MUNGU n.k.

Hayo yametimiza kipengele cha njozi ya Yesu ya jiwe kugeuza mkate.

(7) KUJITUPA KWA MAKUSUDI KUTOKA JUU YA KINARA.

Kujitupa kwa makusudi kutoka juu ya kinara kutegemea Mungu Atakuokoa, huko nako ni kukosa kutumia AKILI na ujinga uliofurutu ada ambako hakuwezi kufanywa na mwanadamu yeyote mwenye akili timamu.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Istighfar na Taubah

Kutoka Uk> 3

asili. Ghafar maana yake ni kufunika. Hakuna nabii hata mmoja aliye na nguvu sawa na Mungu, na kwa hivyo hakuna anayeweza kujilinda na kujiokoa, na kwa hivyo wao pia wanahitaji ulinzi wa Mungu, ndiyo maana manabii wote wamefanya istighfar. Pia ni dhana potofu ya Wakristo wanaposema kwamba Yesu hakuwahi kufanya istighfar. Kwa hakika, Yesu (as) alipolia, 'Mola wangu (Eli Eli), mbona umeniacha?' alikuwa, kimsingi, akitafuta rehema na ulinzi wa Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba zaidi alimnukuu Masihi Aliyeahidiwaas, ambaye alieleza kwamba Istighfar ni neno la Kiarabu lenye maana ya kuomba msamaha; kumwomba Mungu akulinde dhidi ya athari mbaya za makosa ya awali ambayo yamefanywa, na awe na ulinzi dhidi ya kufanya makosa au matendo maovu katika siku zijazo. Mtu akimgeukia Mungu, basi Mwenyezi Mungu humuelekea zaidi.

Kukataa Toba Huzuia Maendeleo

Khalifa mtukufuatba aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwaas ambaye alisema kwamba Mwenyezi Mungu anaelezewa kuwa ni Aliye Hai (Al-Hayy) na Mwenye kujitosheleza na anayesimamia (Al-Qayyum). Al-Hayy inarejelea ukweli kwamba Mungu pia hutoa uhai, lakini pia, Hakuuacha uhai aliouumba, kama mwashi anayejenga jengo na kuliacha. Hivyo, ili mtu aendelee kuishi, anahitaji pia istighfar kwa ajili ya nguvu ya kuendelea kuishi na kufanya hivyo bila doa la dhambi.

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba zaidi alimnukuu Masihi Aliyeahidiwaas ambaye alisema kwamba kukataa ukweli wa toba kunazuia maendeleo na mafanikio. Sio siri kwamba mtu katika nafsi yake hajakamilika, kama vile mtu hajazaliwa kuwa mwanachuoni lakini lazima afanye kazi kuelekea hilo. Vile vile, kiwango cha maadili cha mtu kinahitaji maendeleo. Kwa hivyo, hatua za mwanzo za maisha ni zile wakati mtu yuko chini ya matamanio ya msingi na aina za maisha ya kuishi. Ni pale mtu anapotambua hali hii duni na kutoka ndani yake ili kumkaribia Mungu, anatubu na kuomba msamaha ili kuwa karibu na Mungu. Hizi kwa ujumla ni hatua ambazo mtu hupitia katika maisha. Ikiwa Mungu hangekubali toba, basi hii ingemaanisha kwamba Hakuwa na nia yoyote ya kutoa wokovu kwa yeyote.

Kukuza Furaha na Kuridhika Katika Maombi

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba alisema kwamba wakati fulani, mtu fulani alimuuliza Masihi Aliyeahidiwaas jinsi ya kuendeleza furaha katika maombi - hili ni jambo ambalo watu wanauliza hata leo. Masihi Aliyeahidiwaas alisema kwamba inakuja kwa njia ya matendo mema, na kuomba kwa Mwenyezi Mungu kuendeleza furaha hii kwani haiwezi kuendelezwa bila msaada Wake. Vile vile, mtu lazima aendelee kwa kudumu. Hata hivyo, ikiwa mtu hatajitahidi katika suala hili, basi hawezi kufikia kile anachotafuta. Bila neema ya Mungu, mtu hawezi kufikia chochote, na hivyo mtu anapaswa daima kutafuta neema na msaada Wake. Mtu anayekuwa mbali na Mungu anakuwa kama shetani. Kwa hivyo, mtu anapaswa kutafuta msamaha kila wakati, ili aweze kuokolewa kutoka kwenye uharibifu.

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwaasambaye alisema kwamba milango ya neema ya Mungu haifungwi kamwe. Ikiwa mtu ametubu kweli, basi ajue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na kurehemu. Mtu asifikiri kwamba Mungu atawasamehe baadhi na wengine hatowasamehe kwani kufikiria hivyo ni aina ya kutomheshimu Yeye, kwa sababu rehema ya Mungu ni kubwa, na mlango wa rehema Yake haujafungwa kwa yeyote.

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwaas ambaye alisema kwamba ili kuleta mabadiliko katika nafsi ya mtu, ni lazima atake msamaha. Wale wanaotoa kisingizio kwamba wanashughulika sana na kazi zao za kidunia ili wawe makini kumgeukia Mungu na kuomba wanapaswa kuwa waoga. Wanapaswa kuzingatia hili. Kwa kweli, ikiwa mtu angeomba ruhusa kutoka kwa mwajiri wake, basi katika hali nyingi, angepewa. Toba ya kweli na kutafuta msamaha inaweza tu kuzaa matunda wakati amri za msingi za ibada zinafuatwa.

Hadhrat Khalifatul Masih Vatba aliomba kwamba tuweze kuelewa roho ya kweli ya toba na kutafuta msamaha na tuwe wale wanaotubu kikweli na kuomba istighfar.

Sala ya Jeneza Huzur Aqdasatba alisema kwamba ataongoza sala ya Jeneza ya ghaib kwa marehemu wafuatao:

Ansa Begum

Ansa Begum ambaye alikuwa binti wa Mir Muhammad Ishaq. Alizaliwa Qadian. Jina la mama yake lilikuwa Saliha Begum. Ameacha watoto wawili wa kiume na wa kike. Daima angeitumikia familia yake kwa njia kuu. Alikuwa Ahmadiyya mwaminifu mwenye tabia rahisi na ya upendo. Alikuwa anaifahamu vyema historia ya Jumuiya. Mara nyingi alishauri watu kuishi kwa maisha ya heshima. Alikuwa na huruma kubwa kwa wanadamu. Alikuwa na shauku ya kutumikia imani. Mara nyingi alikuwa akisafisha msikiti huko New York. Khalifa mtukufuatba alimuomba Mwenyezi Mungu awawezeshe watoto wake kuendeleza urithi wa wema wake, na amjaalie msamaha na rehema.

Bushra Akram

Bushra Akram wa Sialkot. Alikuwa mwema na mchamungu. Alikuwa mkarimu, mwenye huruma kwa maskini na alipenda Ukhalifa. Ameacha mumewe, watoto watatu wa kike na wa kiume. Mwanawe ni mubashir nchini Sierra Leone na hakuweza kuhudhuria mazishi kwa sababu ya kuwa katika utumishi. Ingawa alikuwa na mwana mmoja tu, alisema kwamba hata kama angekuwa na wana saba, angewatoa wote kwa huduma ya imani. Maneno yake ya mwisho kwa mtoto wake yalikuwa kuwa mvumilivu na thabiti. Khalifa mtukufu (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu amjaalie maghfira na rehema na awape subira watoto wake.

Musarrat Jahan

Musarrat Jahan wa Australia. Babu yake alikuwa Sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Alikuwa amelazwa kwa miaka 16 baada ya kuvuja damu kwenye ubongo. Alikuwa makini kwa Sala za kawaida na alikuwa mahali pa powekwa wakfu nyumbani kwake kwa ajili ya kusali. Aliipenda sana Khilafat. Ameacha mumewe, wana watatu na binti watatu. Mwanawe mdogo Hafiz Rashid Javaid ni Nazim Darul Qadha Rabwah. Khalifa mtukufu (atba) alimuomba Mwenyezi Mungu amjaalie rehema na msamaha na awawezeshe watoto wake kuendeleza urithi wa wema wake.

Nasir Ahmad Qureshi

Nasir Ahmad Qureshi wa Marekani. Ameacha mke, wana wawili na mabinti watatu. Mmoja wa wajukuu zake, Waqas Khurshid ni mubashir, wakati mjukuu wake mwingine anasoma katika Jamia Ahmadiyya Kanada. Aliitumikia Jumuiya katika nyadhifa mbalimbali. Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu amjaalie maghfira na rehema. Alikuwa ameshikamana na msikiti na daima alisimamia mafunzo ya maadili ya watoto wake. Alikuwa ni mtu mwenye msimamo. Khalifa mtukufuatba aliomba kwamba Mwenyezi Mungu awawezeshe watoto wake kuendeleza urithi wa wema wake.

Bustani ya Washairi

Usipange Kukosa Jalsa

Yetu jalsa ya mwaka, wasubiri nini sasa
Je mwakani utafika, Usikose na kuasa
Tabasamu sofanuka, na za kiroho hamasa
Usipange kuikosa, Jalsa ya huu mwaka

Ni mara moja kwa mwaka, siku tatu hesabika
Nuru inayomurika, nyoyo zikatakasika
Madoa ya kaondoka, na neema kufurika
Usipange kuikosa, Jalsa ya huu mwaka

Alianzisha Masiha, kwa mkono wa Mwenyezi
Hudhuri upate jaha, na vyeo vyenyea'azi
Ni kama nyota ya jaha, ama nuru Mbaramwezi
Usipange kuikosa, Jalsa ya huu mwaka

Wallahi natamani, na vyema ninajichanga
Mwaka huu nijewini, nihudhurie Kitonga
Ewe Mola niauni, nisijemwamba kugonga
Usipange kuikosa, Jalsa ya huu mwaka

Aliombea Mahadi, dua kwa wanoshamiri
Kwa sauti ninanadi, nawapa hii habari
Mbinga Pemba Bariadi, tuianzeni safari
Usipange kuikosa, Jalsa ya huu mwaka

Mtunzi..
Sheikh Hussein Ng'amilo.

Wako Wapi?

Yuko wapi Mama Bora, Umi aliyenizaa
Kwa uchungu na subira, mengi alivumilia
Utadhani masihara, ai dunia dania
Nisamehe ya Kahari, yule nilomkosea.

Yuko wapi Mariamu, Mama aliyenilea
Kanilea kwa nidhamu, ni muhimidi jalia
Na funguo za elimu, ni yeye kanipatia
Rabi mpatie fungu, pale Janati. Nainu

Yu wapi haji Shabani, Baba yangu wa haiba
Na pale kwetu nyumbani, katulea kwa mahaba
Pasi shida asilani, tunakula na kushiba
Kapumzike Katoro, palipo kitovu changu.

Yu wapi Baba Rajabu, Rajabu wa Hamsini
Alinipenda ajabu, Mapenzi toka rohoni
Namuombea wahabu, apate kiti peponi
Pale walipo watawa, na walioteuliwa

Abudala Shaabani, kutwa anatabasamu
Furaha tele usoni, kwa sisi ndugu wa damu
Msamehe ya Manani, apate yote naimu
Hakuna wa kusamehe, ila ni wewe Rabana.

Yahaya wa Shaabani, Rubani wetu Azizi
Wa ndege yetu angani, kaongoza kwa ujuzi
Amelala Akisoni, walipolala wazazi
Twaomba apumzike, kwa salama na amani.

Yu wapi kaka Badiru, alinipenda kwa dhati
Kitu chake kwa uhuru, akanipa bila hati
Sina ila kushukuru, Mapenzi yake kahari
Sisi wa mola Jalia, na kwake tutarejea.

Tamo somo ndugu zangu, kwamba nami taondoka
Kulipata fungu langu, toka kwa mola Rabuka
Rabi epusha machungu, nije kwa kuheshimika.
Na nyuma niache jina, lisilokuwa na doa.

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani.

Umlinde wetu Mwana

Sifa njema nizakwako, ulotupatia mwana
Maombi twatumakwako,umlinde wetumwana
Asijekutoka kwako, Dunia akiiona
Umlinde wetu mwana, tunakuomba rabbana

Masiruri lakejina, twaomba uliridhie
Mwenyefuraha kijana, twaomba mjaalie
Asiwe wakujiona, upole mjaalie
Mpe furaha kijana, Wengine awagawie

Malezi umpatie, akili umtanue
Ujinga autambue, wongofu aushikie
Haki aing'ang'anie, batili aichukie
Umlinde wetu mwana, tunakuomba rabbana

Mwezimei kumi tatu, Jumamosi alasiri
Efu mbili shina tatu, Mgeni aliwasiri
Kuzizima hofu zetu, furaha katuajiri
Wewe nifuraha yetu, masiruri Masihi.

Twakushukuru manani, wema unatutendea
Tuimarishe Imani, dini kuitumikia
Namalezi yaimani, mwana kumjaalia
Umlinde wetu mwana, tunakuomba rabbana.

Mtunzi
Masihi Omary Stambuli Kisagwa

KASIDA

...Kutoka toleo lililopita

9. إِنِّيْ أَرَى فِيْ وَجْهِكَ الْمُتَهَلِّلِ
شَأْنًا يَّفُوْقُ شَمَائِلَ الْإِنْسَانِ

Kwa hakika naona katika uso wako ung'aao shani inayoshinda sifa njema za binadamu wote.

10. وَ قَدِ اقْتَفَاكَ أُولُو النُّهٰى وَ بِصِدْقِهِمْ
وَدَعُوْا تَذَكُّرَ مَعْهَدِ الْأَوْطَانِ

Na bila shaka wenye busara wamekufuata, nao wameacha hata kukumbuka watani wao kwa sababu ya uaminifu wao.

11. قَدْ اٰثَرُوْكَ وَ فَارَقُوْا أَحْبَابَهُمْ
وَ تَبَاعَدُوْا مِنْ حَلْقَةِ الْإِخْوَانِ

Bila shaka walikutanguliza na kuwaacha marafiki zao, na kutengana na ndugu zao.

12. قَدْ وَدَّعُوْا اَهْوَاءَ هُمْ وَنُفُوْسَهُمْ
وَ تَبَرَّءُوا مِنْ كُلِّ نَشْبٍ فَانِ

Walijitanga na matamanio yao na nafsi zao, na waliondokewa na hamu ya miliki yenye kuangamia.

13. ظَهَرَتْ عَلَيْهِمْ بَيِّنَاتُ رَسُوْلِهِمْ
فَتَمَزَّقَ الْأَهْوَاءُ كَالْأَوْثَانِ

Dalili bayana za Mtume[saw] wao zikawadhihirikia, basi tamaa zao zikavunjika tikitiki kama masanamu.

14. فِيْ وَقْتِ تَرْوِيْقِ اللَّيَالِيْ نُوِّرُوْا
وَاللهُ نَجَّاهُمْ مِّنَ الطُّوْفَانِ

Katika wakati wa giza la mausiku wakaangazwa, na Allah Akawaokoa katika tufani.

15. قَدْ هَاضَهُمْ ظُلْمُ الْأُنَاسِ وَ ضَيْمُهُمْ
فَتَثَبَّتُوْا بِعِنَايَةِ الْمَنَّانِ

Bila shaka dhulma za watu zikawaponda sana, lakini wakasimama kidete kwa rehema ya Manani.

Kitabu cha KASIDA
Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Kasida ya kumsifu Mtume Muhammad[saw]

...Kutoka toleo lililopita

22
حتى انثنى برٌ كمثل حديقةعذب الموارد مثمر الأغصان

Tafsiri:
Hata pori zikageuka kuwa kama viunga vyenye chemchemi tamu na matawi (ya miti) yenye matunda.

Maelezo:
Katika ubeti huu hali ya maisha ya masahaba kabla ya kujiunga na Uislamu imeelezwa kama pori kusiko na ustaarabu. Baada ya kuongoka maisha yao yaligeuka kama bustani ambako chemchemi za maji matamu ya kiroho zinabubujika na kurutubisha miti inayozaa matunda mengi. Miti na matunda ya Kiislamu ni watu ambao bado wanaendelea kupata nguvu kutoka mafundisho ya Uislamu na kuyasambaza duniani.

23
عادت بلاد العرب نحو نضارةبعد الوجى والمحل والخسران

Tafsiri:
Mataifa ya kiarabu yakaelekea kustawi baada ya hali ya ukavu, ukame na uharibifu.

Maelezo:
Hali ya Bara Arabu kabla ya ujio wa Uislamu ilikuwa mbaya sana. Watu walienda mbali sana na dini na walizidi katika madhambi na maovu. Uharibifu wa kila aina ulienea na ukapelekea maji ya kiroho kukauka au kukosekana. Katika hali kama hii ikaja dini tukufu ya Uislamu na watu wakaona mabadiliko katika hali zao za kidini. Kwa kweli ustawi ukapatikana.

24
كان الحجاز مغازل الغزلانفجعلتهم فانين في الرحمان

Tafsiri:
Watu wa Hijazi walikuwa ashiki wa wanawake warembo, nawe ukawafanya wakijipoteza katika Rahmani

Maelezo:
Kabla ya ujio wa Uislamu, watu wengi walizama katika mambo mabaya. Mtume Mtukufu[saw] aliwaelekeza na kuwafundisha kwamba Mungu ni mmoja apaswaye kuabudiwa; ambaye ni mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu; ambaye ni mtoaji wa riziki; aondoaye shari zote na aletaye heri zote. Hivi twapaswa kumwabudu Yeye pekee na kutekeleza maamrisho yake.

Shahabu Ahmad
Morogoro
Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Sungura na Kobe

Sungura alikuwa akimdhihaki kobe siku moja kwa kuwa na mwendo wa kigoi goi.

"Hivi huwa unafika mahala popote?" aliuliza kwa kicheko cha kebehi. "Ndio," alijibu kobe, "na nitathibitisha fikra yako hiyo potofu. Ninakwenda kushindana mbio na wewe na kukuthibitishia."

Sungura alifurahishwa sana na wazo la kushindana mbio na kobe, isipokuwa kwa raha ya kigezo cha makubaliano naye. Kwa hiyo mbwa mwitu, ambaye aliazimia kuwa mwamuzi, aliweka alama ya uwanja wa kushindania na kuwaamuru waanze mbio.

Mwanzoni sungura alitoweka kabisa machoni pa watazamaji, na kufanya kobe ajisikie vibaya licha ya kuwa lilikuwa jambo la hovyo kwake kushindana mbio na sungura. Sungura alijilaza pembeni ya mti kupata kausingizi kidogo hadi hapo kobe atakapojaribu kumfikia.

Kobe wakati huo huo akawa anajikongoja bila kukata tamaa taratiiibu tena bila papara, alipita ile sehemu aliyokuwa sungura amelala. Hata hivyo sungura aliendelea kulala kwa amani kabisa; na



alipokuja tu kuzinduka, kobe alikuwa tayari ameshafikia kwenye mstari wa ushindi. Sungura akakimbia kwa kasi zake zote; hata hivyo, hakuweza kumpita kobe kwa wakati muafaka.

Taratibu bila papara hushinda mbio.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

Quran	Hija	Dhambi	Muslih
Saumu	Shawl	Wema	Mauud
Taraweh	Daku	Fasiki	
Ramadan	Futuru	Mwaminio	
Ikhlas	Sihr	Masihi	
Taw	Maombi	Alfazl	

F	F	U	T	U	R	U	N	B	L	D	B	Q	L	Q
T	T	W	E	M	A	M	N	Z	U	T	Z	X	P	D
T	V	A	Q	F	K	M	A	K	H	W	H	K	N	G
F	F	T	R	N	W	F	A	U	X	N	M	I	R	T
S	L	K	L	A	L	D	N	M	U	D	K	H	J	I
H	Y	B	N	A	W	P	Z	T	M	D	T	M	B	A
A	S	A	U	M	U	E	T	A	Q	W	A	M	T	B
W	M	I	F	M	K	L	H	V	B	Q	A	P	R	N
W	A	X	H	Y	R	F	H	S	H	H	V	T	A	L
A	O	M	Y	R	T	L	A	I	D	X	Q	R	M	Z
L	M	A	B	D	X	L	L	S	L	J	U	R	A	B
V	B	S	W	K	H	S	V	Q	I	Q	Y	W	D	D
C	I	I	N	K	U	B	H	X	R	K	J	Y	H	Q
Q	K	H	I	M	K	H	G	X	J	T	I	C	A	M
J	L	I	X	N	M	W	A	M	I	N	I	O	N	H

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Poleni Gazeti la Risala

Na Rajabu Abasi Mkieti
Ikwiriri-Rufiji

Kutoka Uk> 12

Mombasa Kenya Innalillahi wainna ilaihi rajiuni kwani alifariki Aaalim mkubwa katika Afrika mashariki Sheikh Abdillahi Nassir aliyezaliwa huko Mombasa Kenya. Sheikh Abdillahi Nassir naye ni mmoja kati ya watu walitafuta elimu na kuitumikia katika tanzia yake iliandikwa na gazeti la Risala; Toleo na. 112 mhariri ameonesha juhudi za Sheikh katika kutafuta elimu kulimfikisha hadi Zanzibar katika chuo cha Bet -al –Ras Teachars Training College katika miaka ya 1950 na baadae alipo rudi katika nchi ya Kenya alichaguliwa katika baraza la kutunga sharia (Kenya pre-independece Legislative Council) kuanzia 1961 hadi 1963 Sheikh Abdillahi Nassir pia aliwahi kufanya kazi katika shirika la utangazaji la BBC na mashirika mengine mbalimbali baaadae Sheikh Abdillahi Nassir alijiunga na madhahebu ya Kishia baada ya kusoma na kuvutika na mwelekeo huo. Sheikh Abdillahi Nassir naye akafanya kazi kubwa ambayo imeacha alama aliandika vitabu zaidi ya 10 akielezea madhehebu ya shia kwa bahati njema nayeye alijaribu kuogelea bahari yenye kina kirefu kilicho mshinda ndugu yake Sheikh Abdallah Saleh Farsy pale alipoandika kitabu cha kuidogosha na kupotosha ukweli aliokuja nao Hadharat Mirza Ghulam Ahmad[as] mwanzilishi wa jumuia ya waahmadiyya alicho kiita ***Hakika ya Ukadiyani***. Katika kitabu hicho Sheikh Abdillahi Nassir alisukumwa na husda na chuki bila shaka na kuweka uwezo wake wa kielimu kando alioutafuta miaka kadhaa. Sheikh Abdillahi Nassir alipata kusoma vitabu vingi vya jumuia ya Ahmadiyya vya kingereza na Kiswahili ila kwa bahati mbaya amekata shauri na kukataa ukweli. Mwaka 1974 kalamu yenye upanga mkali ilijibu shutuma zote za Sheikh Abdillahi Nassir kwa kutoa kijitabu kwa lugha ya Kiswahili chenye anuani ya ***Ukadiani sio Uahmadiyya***. Maulana Skeikh Muhammad Munawwar H.A akafanya kazi ileile iliyomleta Sheikh Mubaraka Ahmad Afrika ya mashariki ya kuja kusambaza ukweli aliokujanao Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] mwanzilishi wa jumuia ya waahmadiyya. Maulana Skeikh Muhammad Munawwar H.A anaanza kwa kumnukuu Sheikh Abdillahi Nassir kwenye Uk.1 katika kitabu chake hicho cha Hakika ya Ukadiyani "Hatuwaiti Wa-Ahmadiyya kwa sababu ya jina hilo lina maana ya wafuasi wa Mtume Muhammad[saw] ambaye jina lake jingine ni Ahmad kama ilivyo katika aya 7 ya sura 61. Na kwa kuwa wao si wafuasi wa Mtume Muhammad[saw], kama tutakavyoona, ndiyo tukawa hatupendi kuwaita kwa jina hilo." Maulana Skeikh Muhammad Munawwar H.A anashangazwa na tabia hii ya ujeuri kwani anajua fika jina hilo sio la waahmadiyya na anawabatiza jina analopenda yeye. Maulana Sheikh Muhammad Munawwar H.A anamtia darasani mwanafunzi huyu kwa kumuonyesha kuwa unabii kwa hakika unaendelea kwa njia ya Buruuz (yaani mdhihirishaji) akimnukuu Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] mwanzilishi wa jumuia ya waahmadiyya katika kitabu chake cha '***Kuondoa Kosa Moja***' Anasema "Basi, muradi wangu kutoka maandishi yote haya ni huu ya kwamba wapinzani wajinga mananishitaki kuwa 'Huyo mtu anadai kuwa Nabii na Mtume'. Mimi sina madai kama hayo. Mimi siye nabii wala mtume kwa njia wanayofikiria wao. Naam, kwa njia ninayoeleza sasa mimi ni Nabii na Mtume. Basi, yule mtu anishakiye kwa shari kuwa mimi nadai Unabii na Utume ni mwongo na mwenye wazo chafu. Njia ya kuwa Buruuz (yaani mdhihirishaji) imenifanya niwe nabii na mtume; na kwa sababu hiyo mara kwa mara Mungu amenipa jina la Nabii wa Mungu na Mtume wa Mungu"

Maulana Sheikh Muhammad Munawwar H.A anajibu hoja zote na shutuma zilizoletwa na mwanafunzi huyu Sheikh Abdillahi Nassir kwa ustadi mkubwa sana kwa kutumia rejea mbalimbali, Maulana Skeikh Muhammad Munawwar H.A anahitimisha kitabu chake cha majibu kwa kuelekeza mwanafunzi huyu juu ya kutanguliza nia safi katika kutafiti ukweli wa Masih aliyeahidiwa ,Hazrat Mirza Ghulam Ahmad as mwanzilishi wa jumuia ya waahmadiyya. Nionavyo mimi wanachuoni wote hawa wamefanya kazi kubwa lakini ipo kazi moja wameacha kiporo na vifo vyao vinatakiwa vitupe funzo kubwa na kurudi karne kumi na nne nyuma hadi kwa mtukufu Mtume Muhammad[saw] pale alipo sema "Asiye mtambua imamu wa zama zake amekufa kifo cha kijinga" Musnad Ahmad; Jalada 4. Ni masikitiko yangu Maalim Sheikh Aly Basaleh pamoja na mwanchuoni huyu wa kishia Sheikh Abdillahi Nassir walifikishiwa ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa[as] lakini hawakumtambua imamu wa zama. Basi enyi wafuasi na wapenzi wa masheikh hawa na wengine ambao hamja mtambua imamu wa zama nawakumbusheni kwa kunukuu maneno ya Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Akisema "Mimi ndiye yule mjumbe wa Mungu niliyekuja kuleta suluhu katika zama hizi za mwisho. Mwenyezi Mungu Amenituma pamoja na ishara zisizopungua elfu kumi, Amenifanya Bwana Yesu kwa wakristo, Krishana kwa Wahindu, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi kwa Waislamu." Basi njoo waja wa Mungu kwa malaki na maelfu mjiunge na jumuia hii ya iliyoundwa kwa mwongozo maalum wa Mungu kwa kumtuma Masihi na Mahdi katika zama hizi za mwisho. Tembelea tuvuti yetu ya; www.alislam.org.

Shule ya Msingi Ahmadiyya wafanya Mahafali ya Wahitimu wa Darasa la Saba

Kutoka Uk> 5

usomaji wa Kurani tukufu na kufuatiwa na wimbo wa taifa na wimbo wa shule.

Kisha ilifuata ripoti ya shule, na ripoti hiyo ilionyesha kuwa shule hii ilianzishwa mwaka 2014 na inapakana na eneo (uwanja) la Jamia Ahmadiyya ,hivyo baadhi ya majukumu yamesimamiwa na mkuu wa chuo kwa kusaidiwa na baadhi ya waalimu wa Jamia.Ripoti hiyo pia inaonyesha kuwa shule ina vyumba 10 vya madarasa na 3 vya utawala kwa maana ya ofisi n.k. Sambamba na hilo, shule pia ina vyoo vya kisasa na ukumbi mkubwa uitwao Masroor Hall.

Ripoti pia inaonyesha kuwa shule inatoa elimu bora na kwa gharama nafuu kulinganisha na shule nyingine zote.Zaidi ya hayo,asilimia 33 ya wanafunzi wanapata punguzo la ada.

Jumla ya wanafunzi 21 wanatarajiwa kufanya mtihani wa darasa la saba mwaka huu na hivyo kufanya jumla ya wahitimu wa elimu ya msingi kutoka shule ya msingi Ahmadiyya kufikia vijana 70, baada ya ripoti ya shule,mgeni rasmi aligawa zawadi ya vyeti kwa wahitimu.

Waalimu na wafanya kazi mbalimbali wa shule nao pia walipatiwa zawadi maalum. Baada ya hapo,mheshimiwa mgeni rasmi alipata fursa ya kutoa nasaha kwa wahitimu ,na katika nasaha zake mheshimiwa Amir sahib aliwahimiza wahitimu kuendelea kudumisha nidhamu kwa waalimu wao na viongozo mbalimbali na kwamba wawe ni wenye faida katika jamii. Aliendelea kusema kuwa Jumuiya imekuwa ikitoa huduma muhimu katika jamii kwenye nchi mbalimbali kwa lengo la kuhudumia kwa lengo la kupata radhi ya Allah.

Aidha aliwaasa wahitimu kwamba wazidi sana kumwomba msaada Mwenyezi Mungu ili wapate mafanikio na ufahamu katika mitihani yao.Mwisho Amir sahib aliongoza maombi ya kimya na hafla ilihitimishwa kwa wanafunzi,waalimu na wageni waalikwa kupatiwa viburudisho.

Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Kutoka Uk> 2

Mtume Mtukufu[saw] kwa kuelekeza uso wake upande wa Yemeni alikuwa anasema kuhusiana na Owais Karni[ra] kwamba mimi ninasikia harufu ya Mungu kutoka Yemeni. Pia, alikuwa anasema kwamba yeye (Owais) anashughulika na kumtii mama yake na kwa sababu hii hawezi kunifikia mimi. Kidhahiri, jambo ni hili kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwapo lakini yeye hakuweza kumwona kwa sababu tu ya kujishughulisha kikamilifu katika kumtumikia mama yake. Lakini mimi naona kuwa Mtume Mtukufu[saw] alisisitiza kutoa salamu hususani kwa watu wawili tu; ama kwa Owais au kwa Masihi basi; hili ni jambo la ajabu ambalo wengine hasa hawajaweza kushirikiana nalo, mimi ninawaambieni kwelikweli kuwa watu ambao hawajali wazazi kamwe hawatapata heri yoyote."

(Malfuzat, juz. 1, uk. 295-296)

MATUKIO KATIKA PICHA













Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka toleo lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 8



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Siku moja tarehe 28.12.2018 majira ya adhuhuri hivi nikiwa njiani natokea mkoani Tabora mjini katika kufunga na kuhitimisha kambi ya malezi kwa Majlis Khuddamul Ahmadiyya (Nikiwa ni Naib Sadr Kanda ya Ziwa), nilipokea simu kutoka kwa Naib Amir Tarbiyyat na Tabligh (wakati huo) maulana Sheikh Bakri Abeid Kaluta sahib. Simu ambayo ilikuwa ni taarifa na agizo kwangu kuwa nijiandae siku inayofuata basi niwe jijini Mwanza kwa ajili ya kumpokea kiongozi wetu huyu akianza ziara rasmi ukanda wa Ziwa, nami nikaitikia kwa utiifu wa “naam kusikia na kutii”. Hapo nilikuwa nimeshatumia takriban siku 4 za hekaheka kuitumikia Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya mkoani Tabora na sijapumzika, nipo njiani natakiwa kuunganisha kazi nyingine kwa mwezi mzima kuitumikia Jamaat ul Ahmadiyya tena.

Nikiwa tayari nimetoa taarifa nyumbani kwangu Kahama ya kwamba nipo njiani narudi na nitapumzika wiki nzima kwa uchovu wa majukumu ya kijamaat, nikapata ugumu tena kumwambia mke wangu kuwa leo narudi nyumbani Kahama ila kesho natakiwa kusafiri kwenda Mwanza na sitokuwepo nyumbani kwa majuma kadhaa. Nikajisemea hapa nisipige simu, bali nikifika salama Kahama basi ndio nimweleze mke wangu juu ya hii safari nyingine iliyobeba uzito wa kiongozi wetu namba mbili kijamaat nchini Tanzania. Naam nikafika nyumbani na baadae nikamweleza, mke wangu akanielewa. Akaniambia “yote kheri ilimradi unamtumikia Allah haina shida” wewe jitoe tu mume wangu. Kisha akanitayarishia nguo zangu tayari kwa safari kesho yake.

Akiwa anatumikia nafasi nyeti ya Naib Amir wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania (Mahubiri na Malezi), maulana Sheikh Bakri Abeid Kaluta sahib alifanya ziara ya mwezi mmoja Ukanda wa Ziwa. Mipango ya ziara hii ilijumuisha mikoa ya Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara, Simiyu, Geita na Tabora. Hii ilikuwa ni ziara ndefu sana iliyohusisha kusafiri usiku na mchana bila kuchoka, na kufanya kazi usiku na mchana pasipo kuchoka. Maulana Sheikh Bakri sahib aliambatana na msaidizi wake (Katibu wa ziara hii) kijana ndugu Ismail Abdul Nasib sahib, kijana hodari mno na asiyechoka kutekeleza majukumu ya kwa kazi yake hiyo aliyokabidhiwa na Naib Amir sahib.

Maulana Sheikh Bakri Sahib alisafiri kwa bus akiwa na ndugu Ismail Abdul Nasib (Prof. Chikunde) kutoka Morogoro mpaka Mwanza, walifika usiku jijini Mwanza na kupokelewa na ndugu Yusuf Mgeleka Sahib aliyesafiri kutoka Kahama kuja kumpokea Naib Amir sahib kwa ajili ya kuungana nae kwenye ziara yake hii muhimu. Kisha baadae alilakiwa na Sheikh wa Mkoa wakati huo Maulana Sheikh Waseem Ahmad (ambae hivi sasa yupo Uingereza). Na kwa siku zote alizokuwepo Mwanza, Sheikh alikarimiwa huduma zote nyumbani kwa ndugu Yahya Kambaulaya kupitia mkewe, maana ndugu Yahya alikuwa safari ya mbali kikazi. Sheikh wa Mkoa wa Mwanza pia alihudhuria nyumbani kwa bwn Yahya kwa ajili ya chakula cha jioni kilichoandaliwa kwa mapokezi ya Naib Amir sahib.

Ziara ilianza kwa kuutembelea mkoa wa Geita, na tulijaaliwa kupata usafiri wa bus ambapo bwn Mohamed Amir wa Mwanza alitusaidia kupata ticket kwa ajili ya safari. Safari ilianzia Mwanza nyegezi Mnamo saa 12:05 Asubuhi kuelekea Geita ambapo safari ilipitia ferry/kivuko cha Mv Busisi kilichopo katika Ziwa Victoria. Sote watatu tukasafiri alfajiri kutoka Mwanza na kuelekea mkoa wa Geita, na tulifika Geita mjini majira ya saa tatu asubuhi. Tulipofika pale Geita mjini, maulana Sheikh Bakri sahib akasema ngoja tuanzie hapa tumsalimie mpwae anayefanya kazi katika mgodi wa GGM yaani Geita Gold Mine (Ashanti) bi Ashura Dunia. Tulikutana nae mjini na baadae akatukaribisha nyumbani kwake ili kupajua, baada ya nusu saa ziara ikaanza kuelekea kijijini Nungwe yalipo makao makuu mkoani Geita. Nakumbuka tulikodi gari ndogo kutoka mjini mpaka Nungwe. Tulifika Nungwe Jamaat na kupokelewa na Mwl Ramadhan Mahmood sahib aliyekuwa anasimamia mkoa huo mpaka hivi leo. Mnamo saa 06:12pm mchana tuliwasili katika Tawi la Nungwe. Mnamo saa 06:30 mchana kikao kilianza kwa usomaji wa Qur an tukufu na khadim wa Nungwe kisha yalifuata maombi ya pamoja yaliyoongozwa na Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat kisha lilifuata shairi na usomaji wa Viapo Vilivyoongozwa na Qaid wa mkoa Geita.

Tukiwa pale Nungwe basi Naib Amir sahib Maulana Sheikh Bakri sahib ndipo alipoanza rasmi kuwasilisha yaliyomleta na kujionea kwa wanajamaat wenyewe, na tukasali swalat dhuhr pale Nungwe. Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat alitoa hotuba kuhusu Makusudio na Matarajio ya Jumuiya ya Ahmadiyya kwa khadim wa tawini. Baadae tulitumia usafiri wa pikipiki kuzielekea Jamaat zote zilizopo mkoani Geita mpaka jua kuzama, na tulifanikiwa. Kwa maeneo yote hayo Naib Amir sahib alikuwa akitoa nasaha nyigi sawa na azma yake, nasi tukimsaidia.

Nikiwa nae bega kwa bega katika ziara hii, ama kwa hakika nilishuhudia jihadi kubwa sana aliyoifanya maulana Sheikh Bakri sahib katika kuzitembelea hususan jumuiya hizi nyingi zikiwa ni changa na wanajumuiya wake wachanga. Ziara yake Naib Amir sahib ilijikita katika mambo kadhaa na nitayaeleza sawa na muda wangu unavyoniruhusu.

1. Kujiridhisha uhai wa Jumuiya na wanajumuiya wake.
2. Kuhimiza mahubiri na malezi kufanyika kwa nguvu zote.
3. Kutoa elimu na kuandaa mbinu za kiuchumi kwa wanajumuiya wake kupitia ufugaji wa kuku.
4. Kukuza vipato kwa wanajumuiya na kuhamasisha kuongeza watoaji wa michango kupitia ufugaji wa kuku.
5. Kuhimiza mahubiri kwa majirani zetu wanaotuzunguuka, na wanaozunguka misikiti yetu (mahubiri ya nyumba kumi kumi).

Hii ilikuwa ni kazi kubwa, tena kubwa sana kufikisha jumbe hizo kwa wanajamaat wengi ambao ni wapya huku usukumani. Ikumbukwe ziara hii ilifanyika nyakati za masika ambapo kilimo kimepamba moto na mvua zikinyesha kwa wingi sana, jambo ambalo kwa mila za watu wa Kanda ya Ziwa ni kwamba, mvua zinaponyesha basi kipaumbele chao ni kilimo. Jamii yote ya Wasukuma kwa maana ya familia nzima, huwa mashambani na mbugani, jamii hii hawana masihara na suala la kilimo kujipatia chakula.

Katika Mkoa wa Geita, Naib Amir sahib alitembelea matawi ya Nungwe, Mwenegezi, Nyamwilolelwa, na Kabugozo Jamaat. Kwa nyakati zote hizo, matawi yote ilikuwa ni nyakati za masika.

Kwa kuwa mie (msimuliaji) ni mwenyeji wa ukanda huu na mzoefu wa mila za huku, nikawaza juu ya ufaulu wa ziara hii sawa na mazingira ya nyakati husika, nikawaza je tutafaulu kuwapata wanajamaat (ambao bado ni wachanga) waache kazi zao siku nzima na kuja kumsikiliza Naib Amir sahib na ujumbe wake? Nikajisemea, kwa kuwa hii ni kazi ya Allah basi tutafaulu Insha Allah. Kumbe wakati najiuliza swali hilo, nae Naib Amir sahib alikuwa akijiuliza swali hilo hilo pia. Nakumbuka maulana Sheikh Bakri sahib akatuambia (mimi na bwn Ismail Nasib) kuwa tufanye maombi sana ili ziara ipate ufaulu, na akatuhimiza kuwa yeyote atakayepata njozi basi atusimulie ili tupate muongozo kwa tunayoyaelekea. Basi tukafanya hivyo na mmoja wetu (bwn Yusuf Mgeleka) akapata njozi fulani ambayo ilimchukua muda mrefu kutafakari kabla ya kuisimulia kwa Naib Amir sahib na pia kwa bwn Ismail. Baada ya njozi hiyo, basi ziara ikawa ni nyepesi, yenye ufaulu mkubwa na ambayo haikuingia dosari ya aina yoyote ile mpaka mwisho wake, Alhamdulillah. Usiku tulirudi Geita mjini na kulala, siku hiyo tulialikwa nyumbani kwa bi Ashura Dunia kwa mapumziko yetu.

Asubuhi majira ya saa tatu tulielekea stendi ya Mkoa kwa ajili ya kupanda bus kuelekea Mkoani Kagera, na tulifaulu kupata bus ambayo ilitokea Mwanza kwenda Bukoba. Tulianza safari ya bus mpaka Bukoba mjini, pale Bukoba mjini tulipokelewa na marehemu mzee Omar Bishazo, Mwl Issa Malenge Sahib na wanajumuiya wengine. Na moja kwa moja tulienda kupumzika kwa muda katika lodge ya marehemu mzee Omar Bishazo (Allah amrehemu). Baada ya mapumziko mafupi na chakula, tulienda Makao Makuu ya Jamaat mkoani Kagera maeneo ya Katoma na Naib Amir sahib alilakiwa na wanajumuiya wa pale. Tulisali na baada ya sala basi semina maalum ilianza mpaka usiku, baada ya swalat I’shaa tulirejea kwa mapumziko kule lodge. Sisi hatukujali kabisa habari za mwaka mpya, sherehe zake na mengineyo zaidi ya kumtumikia Allah pekee katika ziara hii.

Mapema asubuhi ilikuwa ni kuelekea kijijini Kagenyi kupitia Karagwe mjini na tuliambatana na Dr Jamil Bishazo kwa kutumia gari yake, tulifika Kagenyi majira ya saa sita na kulakiwa na wanajamaat wa pale wakiongozwa na mzee Abdulrahman Nyamihasi na Mwl Musa Kaswezi sahib. Tulikaribishwa kwa chai, na ndipo semina ya siku moja ikaongozwa na kuhitimishwa na Naib Amir sahib mwenyewe, ujumbe ukiwa ni ule ule alioanza nao mkoani Geita. Kwa kweli semina ilifana sana, na jioni majira ya saa kumi na mbili tulianza safari kurudi Bukoba mjini na tulifika usiku kwenye saa tatu hivi tukiwa hoi kabisa. Pale Bukoba mjini usiku huo tulipokewa na mzee Yahya Bishazo tukiwa Katoma na baadae kule lodge tulipokelewa na marehemu mzee Omar Bishazo (Allah amrehemu), tulikula chakula na kupumzika.

Tarehe 03.01.2019 asubuhi na mapema mara baada ya chai, tulienda stendi kwa ajili ya kupanda bus kuanza safari ya kurudi jijini Mwanza na tulifika Mwanza mjini yaani Nyegezi majira ya saa 18:42hrs ya jioni. Tulipokelewa nyumbani kwa bwn Yahya Kambaulaya na kupata chakula na kupumzika kidogo, ambapo saa kumi na mbili jioni tulielekea Markaz ya mkoa wa Mwanza na kupokelewa na Sheikh Waseem sahib. Tulipumzika kidogo na baadae kusali swalat Maghrib na Ishaa, baadae tulirudi kupumzika nyumbani kwa bwn Yahya sahib.

Tarehe 04.01.2019 ilikuwa ni zamu ya wanajumuiya wa Mwanza mjini kukutana kwa semina rasmi na Naib Amir Sheikh Bakri sahib.

Tukiwa kwenye Jamaat za vijijini mkoani Shinyanga hasa kule Ushetu, mvua zilikuwa ni nyingi na gari ilishindikana kupita kwenye njia hizo. Baadhi ya maeneo ikabidi kuacha gari na kutumia pikipiki au baiskeli, mazingira yalikuwa ni korofi sana yakichangiwa na mbuga. Nilimshuhudia maulana Sheikh Bakri akipanda baiskeli ili kuzifikia baadhi ya Jamaat, akipita njia za vichakani na huku akicharazwa fimbo zile za msituni (kwa wanaozifahamu njia hizo), na nilimshuhudia mvua ikinyesha na kulowa kabisa koti lake na kofia akiwa anamtumikia Allah kupitia Jumuiya yake tukufu ya Ahmadiyya. Lakini hali zote hizi hazikumrudisha nyuma Sheikh sahib, bali zilimuongezea jazba kubwa sana ya kuitumikia Jamaat na kushangazwa sana kwa hali na mazingira ya namna Jumuiya ilivyopenya huko vijiji vya mbali sana. Nakumbuka Sheikh Bakri sahib akasema hii ni neema, sasa tunalo jukumu kubwa sana la kufanya malezi kwa wanajumuiya hawa, na huku akiwa na wazo kuona matawi ni mengi sana sasa malezi itakuwaje? Hapo Sheikh sahib akawa na wazo la kutumia sana mitandao ya kijamii katika kuwaelimisha wanajumuiya, akitafakari namna ya kupata urahisi wa kuwafundisha wanajumuiya katika kuwapa malezi na kuelimika.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Msisimko wa Mahubiri ya Islam

Abdul Imran Mganda

Kutoka Uk> 12

waliyomzunguka kutabasamu na mara nyingine kushangalia. Katika pitapita yake alikwishajijengea mashabiki wengi waliyomuona kijana huyo mwembamba na wala hana kilemba kichwani alivyoweza kuwaangusha Masheikh wenye majina jijini Dar es Salaam. Utamu ulizidi kutokana na uwezo wa Mwl. Abdul Imran wa kujieleza. Kila aliporudi akasali kwanza na mimi nilikuwa miongoni mwa wale waliokuwa na kiu ya kusikiliza hayo ambayo alikuwa akieleza. Nilisikiliza kwa makini hoja alizokuwa anatoa. Tukio moja lililotuacha hoi ni lile la Kariakoo lililomuacha Sheikh mmoja maarufu jijini Dar es Salaam. Sheikh Nurudini Hussein alipopatwa na kiwewe na kutoka pale akagongwa na gari na kukimbizwa hospitali ya Muhimbili. Kiwewe hicho kilitokana na washabiki wa Mwl. Abdul Imran walipomuona Sheikh Nurudini na kumwambia; Hebu tufafanulie vizuri, huyu anatuambia Nabii Isa[as] amefariki, je wewe Sheikh unasemaje? Kwa majivuno na zile mbwembwe walizo nazo masheikh wengi alisema; Naam Qur'an Tukufu inasema Nabii Isa[as] amepita. Bila kuchelewa Mwl. Abdul Imran alimuuliza; kapita kaenda wapi Bagamoyo, Kilwa au Morogoro? Kwa sekunde Sheikh Nurudini alibaki kinywa wazi, kihemea juu! Waliomnusuru ni wanafunzi wake waliosema; twende zetu Sheikh. Huku mashabiki wa Mwl. Abdul Imran wakipiga kelele; jibu swali Sheikh! Ni katika sakata hilo la mashabiki hao na kuvutwa na wanafunzi ndipo Sheikh Nurudini alipogongwa na gari na kupelekwa hospitali ya Muhimbili.

Mwl. Abdul Imran alikuwa akitueleza kwamba wakati wake mwingi wa mahubiri jijini Dar es Salaam hakupata hata nafasi ya kula chakula cha mchana kutokana na watu waliomzunguka wakitaka maelezo na ufafanuzi wa hoja mbalimbali za Jamaat.

Jambo moja ambalo alilifurahia sana Mwl. Abdul Imran ni kwamba kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kila palipokuwa na mkusanyiko wa watu wengi walipatikana mashabiki wa kulinda baiskeli yake.

Elimu yangu nyingi juu ya Jumuiya ya Ahmadiyya nilipata kutokana na mazungumzo yake. Miaka mingi baadaye nilikuja kujifunza kuwa mabadiliko makubwa jijini Dar es Salaam kwa upande wa Islamn yaliletwa na Mwl. Abdul Imran.

Katika jiji la Dar es Salaam katika miaka ya 1960 si watoto, si wakubwa maamkizi yao yalikuwa 'shikamoo'. Ni hwl. Abdul Imran ambaye kwa vitendo kila alipopita penye mkusanyiko na wanaokunywa kahawa au kucheza zumna hao wote aliwapa Assalaam Alaikum na baadhi ya wazee walisema; we kijana huna adabu, hebu tuamkie! Na hapo ndipo Mwl. Abdul Imran alipopata fursa ya kueneza mafunzo ya Islam kama yalivyowekwa katika vitendo na Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Aliwaambia ya kwamba Mtukufu Mtume Muhammad[saw] daima alikuwa anatumia maamikizi ya Assalaam Alaikum na sisi tunatakiwa kumfuata yeye kwani yeye ndiye kigezo chema kwetu.

Kwa kutumia hekima bila kutaka kuumiza hisia za mtu yeyote, Mwl. Abdul Imran aliwaeleza mafundisho ya Islam juu ya usafi na kueleza kuwa maji katika "kulateni' hayakuwa safi. Aliwaambia watu wakaone utumiaji wa bomba katika Msikiti wa Ahmadiyya. Ni kweli baadhi yao walikuja kuona maendeleo hayo. Inabaki kwenye kumbukumbu kuwa Masjid Salaam uliofunguliwa mwaka 1957 ndio Msikiti wa kwanza kutumia bomba kwa ajili ya kutawadha.

Katika mahubiri yake alikumbusha juu ya haki za akinamama kwenda Msikitini kusali. Kablą ya mwaka 1957 hakuna msikiti wowote Dar es Salaam uliyotenga nafasi kwa ajili ya akina mama kufanya ibada. Mwl. Abdul Imran alihubiri na kuwakaribisha Masjid Salaam ili wajionee haki wanayopewa akinamama ya kufanya ibada ya sala.

Ni dhahiri ya kuwa mafundisho ya lslam yalikuwa yametupwa mbali. Mwezi wa Ramadhani kwa Waislam wengi wakishatoka kwenye ibada ya tarawehe ulikuwa ni wakati wa kucheza karata na kupiga gumzo lisilokuwa na maana. Madhumuni ya mazungumzo ilikuwa ni kuvuta muda hadi saa sita usiku ili waweze kula daku. Mwl. Abdul Imran katika mahubiri yake jijini Dar es Salaam aliwaonya Waislam kuachana na mwenendo wa Wayahudi, kwani wao ndio waliokuwa wanakula daku saa tatu usiku. Wengi walipinga jambo hilo na kama kawaida yao wakazomea wakati Mwl. Abdul Imran anahubiri. Ni furaha ilioje kuwa desturi hii kwa kiasi kikubwa hapa nchini imeachwa. Misikiti mingi inatangaza wakati wa kula daku na mwisho wa kula daku. Sawa na majira utasikia wakitangaza kuwa daku ni saa kumi na nusu au saa kumi na moja kasorobo. Jambo hili la kuchelewesha kula daku liliwafanya watu wathibitishe kwa mara nyingine ukafiri wa Ahmadiyya. Kama ni hivyo basi inaonesha Waahmadiyya wamepata wafuasi wengi. Ni mbegu ya Mwl. Abdul Imran aliyopanda na hivi leo tunavuna kwa kufuata mafundisho sahihi ya Islam.

Vitabu alivyotembea navyo Mwl. Abdul Imran katika mahubiri yake ni Qur'an Tukufu na Biblia. Waislam hawakufurahishwa kuona yeye akibeba Biblia. Ilibidi atoe somo juu ya umuhimu wa kusoma kitabu chochote ili uweze kubaini baya na zuri katika kitabu hicho. Islam inaheshimu vitabu vinavyodaiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na inawaheshimu Manabii wote bila kuwabagua. Biblia ni kitabu muhimu chenye mafundisho kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingawaje imekwishaingia mikono ya binadamu katika kitabu hicho, Mwl. Abdul Imran aliwaeleza umuhimu wa kuisoma Biblia na kuielewa kwani licha ya kuingiza mikono yao binadamu kuna ubashiri kuhusu ujaji wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw]. Mafunzo hayo ya Mwl. Abdul Imran yalileta mabadiliko. Hata wauza vitabu waliona wimbi la watu lililokuwa linaulizia Biblia. Biblia nyingi zilinunuliwa na kuanza kusomwa. Makundi mengi ya waislam yaliibuka kufanya mahubiri kwa kutumia Biblia na kuonyesha bishara za ujio wa Mtukufu Mtume[saw] kuonyesha udhaifu wa mafundisho ya Kikristo kutoka kwenye Biblia. Ni kweli kwamba kabla ya Mwl. Abdul Imran ni Waislam wachache waliojishughulisha na Biblia kama wapo. Mabadiliko makubwa yametokea na Waislam hivi leo ni wasomaji wazuri wa Biblia. Ni kazi nzuri aliyoianzisha Mwl. Abdul Imran Sahib.

Jambo ambalo lilimsikitisha Mwl. Abdul Imran Sahib ni hao walioparamia kazi waliyoita kuponda ukristo Mwl. Abdul Imran Sahib yeye alikuwa anahubiri kwa hekima bila kutaka kudhalilisha mtu yeyote, kwa hekima yeye alikuwa akifungua Biblia na kuonesha vifungu bila mbwembwe na majivuno Mwalimu Abdu Imran aliamini wale aliokuwa anawahubiri waliokuwa ni wagonjwa wa kiroho. Daktari hawezi kuwasimanga na kuwakebehi wagonjwa bali ni mchungaji mwema anayetaka kondoo wote warudi zizini bila hata mmoja kuntakuliwa na mbwa mwitu. Miaka mingi wakristo walianza kulalamika na kusema mabingwa wa mahubiri ni Waahmadiyya ambao hawana papara wala hamaki. Aliyefanya wafikie hatua hiyo ya kulinganisha na kutofautisha ni kazi nzuri aliyokuwa amefanya Mwalimu Abdu Imran Sahib.

Mwalimu Abdu Imran ni bingwa hasa wa mahubiri. Haipotei sekunde yake bila kuhubiri. Popote mtakapokuwa mnakwenda, lakini mwisho wake ni mahubiri. Kazi hiyo pia alifanya nyumbani kwake ambapo alijaaliwa watoto wanaopenda kuamini Jumuiya ya Ahmadiyya. Binti yake Radhia anashiriki kikamilifu katika shughuli za Jamati na alifanya juhudi kubwa katika kukamilisha sherehe za Lajna Immaillah kutimiza karne moja. Yeye kwa hivi sasa ni katibu mkuu wa Tanzim hiyo. Mustafa Imran huna haja ya kuuliza ni Mwalimu Abdu Bilhususi katika uwanja wa mahubiri. Kwa ufasaha wa usemaji na uwezo wa kujielezea Mustafa anachokipaji kizuri. Siku moja nimemkuta Kariakoo katikati ya umati wa watu akiwa na ubao wake mkononi. Mambo ya kurudi kiwandani kwake aliyasahau na kuendelea kutoa chakula cha kiroho. Anamapenzi makubwa ya kuhubiri na kuitumikia Jumuiya ya Ahmadiyya. Ni furaha ya Kila mzazi kuona mtoto anafuata nyayo zake.

Mwisho

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 4

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?



HABARI UK> 10

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

Msisimko wa Mahubiri ya Islam

Abdul Imran Mganda

HABARI UK> 11



Hakuna tafrija iliyoleta furaha na uchangamfu kama ile ya Mwl. Abdul Imran Mganda aliporudi kutoka kwenye mahubiri. Wanahistoria wa islam katika jiji la Dar es salaam wanakubali ya kwamba mtu aliyeanza kuleta msisimko wa mahubiri ya dini ya lslam na ufundishaji wa Biblia alikuwa ni Mwl. Abdul imran Mganda. alikuwa ni tafrija ya aina yake na watu Msikitini walisubiri kwa hamu kubwa kurudi kwake na hatimaye maelezo aliyoyatoa kuhusu yote aliyokutana nayo na jinsi gani alivyoweza kutoa maelezo yaliyowafanya

Poleni Gazeti la Risala

Na Rajabu Abasi Mkieti
Ikwiriri-Rufiji

Hivi karibuni tumepokea taarifa ya kifo cha Maalimu Sheikh Aly Basaleh mwanachuoni kubwa katika madhahabu ya Suni wal-jamaa ambaye alitumia muda wa maisha yake katika kuipigania dini tukufu ya kiislamu. Maalimu Sheikh Aly Basaleh alikuwa na kipawa kikubwa sana cha kuongea na kushawishi watu katika majukwaa mbalimbali. Katika shughuli ya msiba wake ambao ulirushwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii sifa zake nyingi njema zilielezwa ambazo kwa hakiki Allah ndiye atakaye mlipa kwa kazi yake hii aliyoifanya kwani alikua msitari wa mbele katika kupigania dini tukufu ya islamu pamoja na waislamu katika hali mbalimbali inasemwa ilitoa michango ya hali na mali kwa vikundi na hata kwa mtu mmoja mmoja hasa kukidhi haja za kielimu na kadhalika Maalimu Sheikh Aly Basaleh amebahatika pia kuandika vitabu kadhaa ikiwamo kitabu cha ''Kwa Nini Waislamu Walalamika'' nikiwa muislamu ni wajibu wangu kusema Innalillahi waina illahirajiuni. Msiba wa maalimu Sheikh Aly Basaleh unanikumbusha msiba mwingine mkubwa ambao ulitokea mwaka jana 11 January,2022 huko

HABARI UK> 8

SYNOPSIS OF RELIGIOUS KNOWLEDGE
(Questions and Answers)

By: **Sheikh Karim-ud-Din Shams**

This booklet covers in summary different topics of Islamic knowledge meant for children who are at school age.

It can also be used by our Mualimeens (religious teachers) during their tarbiyyat classes to Nasirat, Atfal and Khuddams.

MUHTASARI WA ELIMU YA DINI

NA HISTORIA YETU

(Maswali na Majibu)

SHEIKH KARIM-UD-DIN SHAMS

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,250/=

Je, Wajua?

Je wajua kuwa Tesla ni moja kati ya kampuni nyingi zinazotengeneza magari yajiendeshayo yenyewe kutumia Kompyuta. Watu kadhaa wamekutwa wakiwa wamelala wakati gari hizo zikijiendesha zenyewe kwani ni kosa kisheria kufanya hivyo. Kampuni nyingine iitwayo Waymo inatoa huduma ya usafiri wa mjini (Taxi) katika miji kadhaa ya Marekani ambazo hazina dereva (hujiendesha zenyewe). Ni kivutio kwa watu wengi sana kuona wakipanda taxi na kuona taxi ikijingoza yenyewe bila ya dereva.

Wakati tunakwenda mtamboni tulipata habari za kifo cha ndugu yetu - Adam Mpambije. Innalillahi Wainnailaihi Rajiun.

HABARI ZAIDI - Toleo lijalo Insha-Allah

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com